

WAPINDUA
ULIMWENGU
KANUNI ZA KIROHO KUKUANDAA KUWA
MPINDUA ULIMWENGU
KIZUMBA B. NDAGA

# WAPINDUA ULIMWENGU

*"…Watu hawa walioupindua ulimwengu wamefika huko nako."* ***(Mdo 17:6)***

KANUNI ZA KIROHO KUKUFANYA UWE MPINDUA ULIMWENGU

**KIZUMBA BENJAMIN NDAGA**

**©Kizumba Benjamin Ndaga 2025**

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kunakili au kutoa sehemu yoyote ya kitabu hiki kwa kutumia mtambo, mkono au njia nyingine yoyote au kukihifadhi katika mfumo wowote, bila kibali cha maandishi cha mwenye hakimiliki.

**ISBN: 978-9912-43-014-3**

Mwanza, TANZANIA (Afrika Mashariki)

Kizumba Benjamin Ndaga

Simu: +255 697 807 714 / +255 655 857 839

Barua pepe: kizubenjr@gmail.com

Kimepigwa chapa na

Rukilo Printers

+255 762 516 208, rukiloprinting@gmail.com

Mwanza, Tanzania

Jalada la Kitabu: Newtonvisuals

Kimepangwa na kuhaririwa na Bw. Baraka Amosi Petro

## Hitaji la Wapindua Ulimwengu Kizazi Cha Leo

Tunaposema wapindua ulimwengu, ni kizazi cha watu maalumu waliotumwa duniani na Mungu kwa ajili ya kazi maalumu ya kupindua tawala za ufalme wa giza na kusimamisha ufalme wa Mungu kwenye mifumo tofautitofauti ya kiuchumi, biashara, afya, siasa, uongozi, teknolojia, sanaa, burudani, jeshi, dini, mahakama nk.

Katika kurasa za maandiko kuna habari za watu kadha wa kadha wanaume kwa wanawake, wadogo kwa wakumbwa, ambao walitumiwa na Mungu katika mifumo mbalimbali ya ulimwengu kuanzia ikulu, hospitali, uandisi, mahakamani, biashara, burudani, kiroho nk kwa ajili ya utukufu wake. Hebu angalia baadhi yao hapa:

- Luka – Daktari bingwa aliyekuwa na hofu ya Mungu. (Kol 4:14)
- Shidra na Pua – Wakunga(nurses) waliokuwa watumishi wa Mungu. (Kut 1:15)
- Erasto - Wakili mwaminifu wa mji wa Rumi aliyehukumu kwa haki. (Rum 16:23)
- Zena – Mwanasheria mwaminifu aliyeteta wanyonge. (Tito 3:13)
- Zakayo – Mtoza ushuru, mwekezaji, tajiri mkubwa aliyetoa mali zake kuwapa maskini. (Luk 19:8)
- Priscilla & Aquila - Wakandarasi wa nyumba. (Mdo 18:2-3)

- Daudi – Mwimbaji na mpiga kinubi aliyetumia kipawa chake kumtukuza Mungu. (1 Sam 16:18)
- Yusufu – Waziri mkuu wa taifa la Misri. (Mwa 41:41)
- Danieli – Makamu raisi wa taifa la Babeli. (Dan 2:48)
- Sulemani – Profesa wa hekima aliyevuta mataifa kwa hekima yake ya ajabu. (1 Fal 4:34)
- Paulo – Mtume na mwinjilisti wa Kristo aliyehubiri injili pote ulimwenguni. (2 Tim 1:11)

Orodha ni ndefu sana msomaji sitaweza kuwamaliza wote, lakini hii inatuonyesha Mungu alijiwekea watu wake kwenye mifumo mbalimbali ya ulimwengu ili apate kutukuzwa na kuinuliwa mbele za watu wote.

Katika kizazi hiki cha mwisho, Mungu ana mpango mkubwa wa kujiinulia tena wapindua ulimwengu kote duniani ambao atawatumia kwa utukufu mkuu zaidi kwenye mifumo ya ulimwengu kwa lengo kuu la kuharibu hila na kazi zote za adui shetani, huku wakilitukuza na kulisimamisha jina la Yesu Kristo.

*"Sasa ni saa ya hukumu kwa ajili ya ulimwengu huu, sasa mkuu wa ulimwengu huu atatupwa nje." **(Yohana 12:31)***

Haijalishi ushawishi alionao shetani kwenye mifumo ya ulimwengu hivi leo, habari njema ni kwamba saa yake ya kuhukumiwa imefika nayo ni sasa wala sio baadae, ni leo wala sio kesho. Tumekwisha yaingia yale majira ambayo

Bwana wetu Yesu Kristo aliyotutabiria, kwamba adui atakwenda kutupwa nje ya mifumo ya ulimwengu kwa njia ya kizazi cha watu waiitwao *"wapindua ulimwengu."*

Kizazi hiki ni maalumu kutoka mbinguni ni rungu na silaha za vita za Adonai, anazoziandaa katika siku hizi za mwisho kumpondaponda na kumwondoa adui na mawakala wake kwenye mifumo mbalimbali inayoendesha ulimwengu.

**Sifa za Wapindua Ulimwengu**

*i)* ***Ni watu waliotumwa duniani kwa kusudi maalumu la kusababisha mabadiliko.***

*"Palitokea mtu, ametumwa kutoka kwa Mungu, jina lake Yohana."* **(Yohana 1:6)**

Msomaji ni vizuri ukaanza kufahamu Mungu huwa anawatuma watu kuja duniani kwa kusudi lake maalumu, na moja ya sifa kuu ya wapindua ulimwengu ni watu waliotumwa kutoka kwa Mungu duniani kufanya kusudi lake la kuleta mageuzi na mabadiliko yatakayolitukuza jina lake.

Mungu alipokuumba aliweka roho ndani yako yenye kusudi maalumu la kufanya hapa duniani. Kwa hiyo ni vizuri ukatambua kwamba Mungu amekuleta duniani kwa kusudi maalumu la kuupindua ulimwengu kwa ajili ya utukufu wake.